Al-Islam.org
Ahlul Bayt Digital Islamic Library Project
Published on *Al-Islam.org* (https://www.al-islam.org)

Mfungwa wa Allah katika Ardhi!

'Allama Majlisi katika utungo wake mkubwa (kitabu kikubwa) 'The Oceans of Lights' (Bahari za Nuru) anasimulia hadithi ambayo kwayo Mtume (s.a.w.w.) anaombwa kueleza hadhi ya Imamu 'Ali (a.s.) ambapo Mtume (s.a.w.w.) anazungumzia kuhusu fadhila zake kwa urefu sana. Katika nukta moja anasema:

ألا وَمَنْ أَحَبَّ عَلِيًّا سُمِّيَ أَسِيْرُ اللّهِ فِي الأَرْضِ وَ بَاهَى اللّهُ بِهِ مَلاَئِكَتَهُ وَحَمَلَةَ عَرْشِهِ

"Hakika yeyote yule anayempenda 'Ali anaitwa mfungwa wa Allah katika ardhi, na Allah (s.w.t.) hujifaharisha naye karibu na Malaika Zake na wabebaji wa Arshi Yake."1

Hapa nukta mbili lazima zieleweke:

1. Upendo wa 'Ali (a.s.) una maana gani katika hadithi hii?

2. Inamaanisha nini kuwa 'mfungwa wa Allah katika ardhi'?

Kitu gani kinatufanya tumpende 'Ali (a.s.)? Je, ni kwa sababu ya umbo lake lililobarikiwa? Je, ni kwa sababu ya sehemu aliyoishi? Je, ni kwa sababu ya watu aliokutana nao? Je, ni kwa sababu ya kabila lake? Au ni kwa sababu ya tabia zake nzuri, ambazo hudhihirisha Uislamu wa kweli, au katika maneno ya wenye elimu ya kiroho (maurafaa): 'ambayo hudhihirisha Sifa za Mwenyezi Mungu'? Kwa uwazi ni elimu ya udhihirisho wa 'Ali wa sifa za Mwenyezi Mungu ambayo huchochea cheche za mapenzi ndani ya nyoyo zetu. Tungelipenda kufaidi uswahiba wake, bali, kama tungeliangalia jambo lenyewe kwa undani, 'tungelipenda kuwa 'Ali mwingine'. Upendo peke yake humvuta mtu kutafuta umoja na mwenye kupendwa.

Kwa hiyo, waumini ambao wamezoea mapenzi kwa 'Ali (a.s.) kwa kweli hutafuta 'sifa zake'. Na sifa za 'Ali (a.s.) ni sifa za Mtume (s.a.w.w.) na sifa za Mtume (s.a.w.w.) ni Sifa za Allah (s.w.t.). Angalia hadithi ifuatayo kwa uangalifu.

Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) amenukuliwa akisema:

مَنْ أَحَبَّ عَلِيًا فَقَدْ أَحَبَّنِيْ, وَ مَنْ أَحَبَّنِيْ فَقَدْ أَحَبَّ اللَّهَ

"Yeyote yule anayempenda 'Ali, ananipenda mimi, na yeyote yule anayenipenda mimi, anampenda Allah (s.w.t.)..."2

Una maana gani upendo ule ambao hauna athari ya kufuata? Katika hadithi Imamu Muhammad al-Baqir (a.s.) akimhutubia Jabir Ju'fi, anasema:

يَا جَابِرُ مَنْ أَطَاعَ اللَّهَ وَأَحَبَّنَا فَهُوَ وَلِيُّنَا, وَمَنْ عَصَى اللَّهَ لَمْ يَنْفَعْهُ حُبُّنَا ...

"...Ewe Jabir! Yeyote yule ambaye anamtii Allah na anatupenda sisi, ni rafiki yetu, na yeyote yule ambaye anamuasi Yeye (Allah), mapenzi yetu hayatamnufaisha."3

Fikiria kwamba unapenda mno vazi Fulani, ambalo kwa hakika litakufanya uonekane umependeza na mzuri wa umbo. Kama hakuna kizuizi au kuna kizuizi, lakini kinaweza kuondolewa, je, hutajaribu kununua vazi hilo? Kwa hakika utalinunua. Halikadhalika, kama kweli mtu anapenda kupata sifa za Imamu 'Ali (a.s.) na anazo njia ambazo tayari ziko kwa matumizi yake na anaweza kushinda vikwazo vya 'matamanio ya nafsi yake' je, hatajitahidi kuzipata?

Hata hivyo, kuna daraja za upendo, ambazo hubakia katika kiwango cha moyo na zina athari ndogo katika akili na moyo. Watu kama hawa kwa ajili ya kuzihifadhi 'silka ya tabia' zao (fitra) kwa kiwango fulani, watasafishwa katika Moto wa Jahannamu kabla ya kuishi katika Pepo. Baadhi ya hadithi hudokeza ukweli huu.

Lakini kama tukilinganisha upendo wa 'Ali (a.s.) na ufungwa wa Allah (s.w.t.) ambao Allah (s.w.t.) ana fahari nao, ni makosa kufikiria kwamba upendo hapa unasimama tu kwa mhemuko (hisia) wa upendo. Je, kuwa na mhemuko wa upendo kunaweza kuwa sawa na utii kwa Allah (s.w.t.)? Kwa kweli hapana. Kwa hiyo upendo katika hadithi iliyo katika mjadala ni daraja la juu sana. Qur'an Tukufu [2: 165] inadokeza kwenye hili kama ifuatavyo:

وَمِنَ النَّاسِ مَنْ يَتَّخِذُ مِنْ دُونِ اللَّهِ أَنْدَادًا يُحِبُّونَهُمْ كَحُبِّ اللَّهِ ۖ وَالَّذِينَ آمَنُوا

أَشَدُّ حُبًّا لِلَّهِ ۗ وَلَوْ يَرَى الَّذِينَ ظَلَمُوا إِذْ يَرَوْنَ الْعَذَابَ أَنَّ الْقُوَّةَ لِلَّهِ جَمِيعًا

وَأَنَّ اللَّهَ شَدِيدُ الْعَذَابِ

"...Na wale ambao wameamini wanaupendo zaidi sana kwa Allah..."

1. All□ma Majilisi, Bih□r al-Anw□r, j. 27, uk. 115, tr. 89.
2. All□ma Majilisi, Bih□r al-Anw□r, j. 5, uk. 69 tr. 1.
3. Muhammadi al-Rayy Shahri, Miz□n al-Hikma, j. 1, uk.519, tr. 3211.

Source URL: https://www.al-islam.org/fr/node/39636#comment-0